

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA KILIMO



YAH: MABORESHO KATIKA SERA YA TAIFA YA KILIMO YA MWAKA 2013.

SEHEMU YA KWANZA

MAONI/USHAURI KATIKA MABORESHO YA SERA YA TAIFA YA KILIMO YA MWAKA 2013.

Nianze kwa kumshukuru Katibu mkuu wizara ya kilimo na timu yake, kutupatia fursa watanzania na wadau wa kilimo nchini tutoe ushauri na mchango wetu katika maboresho ya sera ya Taifa ya kilimo ya 2013 kupitia tangazo la wizara ya kilimo kwa umma la tarehe 4/6/2019.

Tanzania ni moja ya nchi iliyobarikiwa hapa duniani kuwa na ardhi nzuri na kubwa yenye rutuba ,pia kuwa na vyanzo mbalimbali vya maji na kilimo ni moja ya sekta muhimu katika ukuaji wa uchumi Tanzania , kwa mujibu sera ya taifa ya kilimo ya mwaka 2013 kilimo kiliajiri takribani asilimia **77.5** ya watanzania wote.Kwa muktadha huo kilimo ni tegemeo kubwa katika ukuaji wa uchumi wa Tanzania ya viwanda , kwa sababu malighafi nyingi zinahitajika zitokane na kilimo. Pia kilimo kinaonekana kilichangia GDP(Gross Domestic Product) asilimia **24.1** ,asilimia **30** ya mazao yaliyouzwa nje ya nchi, na wastani wa ukuaji wa sekta ya kilimo kwa miaka mitano (2001-2006) ni takribani asilimia **3.92** na kwa muongo mmoja ukuaji wa sekta ya kilimo toka mwaka 2001-2011 ni takribani asilimia **4.35**, Kutokana na takwimu hizo sekta ya kilimo nchini bado inajikongoja sana,hivyo juhudi zinahitajika sana ili kilimo kiwe na tija nchini.

Huu ni mwaka 2019, ambao ndio umefikia katikati , lakini mwaka huu unasogeza mbele na kutuelekeza tukiwa tumebakiwa na miaka takribani 6, kukamilisha dira ya maendeleo ya taifa mwaka 2000-2025.Katika dira hii

inatuelekeza Tanzania kufikia uchumi wa kati na kutoka kundi la nchi maskini duniani ifikiapo 2025.

Kichecheo kikubwa cha kutupeleka uchumi wa kati, kwa kuboresha hali ya uchumi wa taifa na Tanzania ya viwanda, kama inavyohubiriwa katika sehemu mbalimbali za nchi, jambo ambalo ni zuri na la kutia faraja na matumaini.

Neno, Tanzania ya viwanda limeanza kupata umaarufu, wakati wa kampeni za uchaguzi mkuu mwaka 2015, ni sera nzuri sana na yenye kutia matumaini kwa wale wote wanaofahamu umuhimu wa viwanda katika ukuaji wa uchumi, katika taifa lolote lile.

Hivyo basi sekta pekee ambayo itachagiza kwa kiasi kikubwa Tanzania ya viwanda ni **KILIMO**. Nchi mbalimbali hasa za bara Asia na Ulaya ambazo zilikitumia kilimo katika maendeleo jumuishi na hatimae kufanikiwa katika azma yao ya mapinduzi ya viwanda. Nimeamua kutumia ulinganishi huu kwa sababu kuu moja nchi za Asia kama China, Indonesia, Malaysia, Vietnam na sasa Cambodia ni nchi ambazo wakati tunapata uhuru tulikuwa nazo sawa kiuchumi lakini kwa sasa wao wametuaacha mbali, hivyo tuna haja ya kujifunza kwao kwa namna walivyofanikiwa na hatimaye sisi tutumie baadhi ya mbinu zao katika mazingira ya nchi yetu.

Mchango wangu utajikita katika maeneo yafuatayo,

1. Umwagiliaji (irrigation)
2. Utumiaji wa zana za kilimo (Mechanization)
3. Ushirika (Cooperatives)/Masoko (Markets)

Haya ni maeneo ambayo mchango wangu utajikita katika maboresho ya sera ya taifa ya kilimo ya mwaka 2013.

1. Umwagiliaji (Irrigation)

Kwa mujibu wa sera ya umwagiliaji ya mwaka 2010, inaeleza kwa kina katika kutilia mkazo kilimo endelevu cha umwagiliaji kwa kuhakikisha maji yanapatikana kwa ajili ya umwagiliaji, ujengwaji wa skimu za umwagiliaji na kutilia mkazo teknolojia zote za umwagiliaji nchini, lengo likiwa ni kuongeza uzalishaji wa mazao, kuhakikisha kunakuwa na akiba ya kutosha ya chakula nchini na kupunguza umaskini uliotopea kwa watanzania hasa wa vijijini.

Katika sera ya umwagiliaji inatilia mkazo pia ushirikishwaji wa sekta binafsi katika Uwekezaji katika kilimo kwa njia ya umwagiliaji.

Kwa mujibu wa takwimu za wizara ya kilimo na sera ya kilimo ya taifa ya mwaka 2013 Tanzania ina ardhi yenye rutuba yenye kufaa kulimwa yenye ukubwa wa takribani hekta **milioni 7.1** lakini eneo linalolimwa kwa umwagiliaji ni takribani hekta **331,490** ambayo ni sawa na asilimia **3.9** tu. Hii ina maanisha kwamba bado kuna changamoto nyingi za kukifanya kilimo cha umwagiliaji kukwama , baadhi ya changamoto hizo ni upungufu wa wataalam(wahandisi na technicians), bajeti kiduchu, ukosefu wa elimu kwa wakulima, muundo wa tume ya umwagiliaji usio rafiki kwa wakulima n.k

1.1 Maoni/Ushauri

Umwagiliaji ni namna ya kutumia maji katika mimea kwa muda na wakati sahihi ,husaidia ukuaji mzuri wa mazao , kuondoa utegemezi wa mvua , kuongeza uzalishaji wa mazao, kudhibiti magugu, kudhibiti Mmonyoko wa udongo na uhakika wa kuvuna.

Wahandisi wa kilimo na umwagiliaji

► Kutokana na umuhimu wa umwagiliaji, mwaka 2011 serikali ilianzisha fani ya Uhandisi wa umwagiliaji na rasilimali watu (Bsc. Irrigation and water resource engineering) katika chuo kikuu cha Sokoine cha kilimo(SUA) ili kuongeza nguvu katika fani kongwe ya Uhandisi kilimo(Bsc. Agricultural Engineering) ambayo kwa sasa inatolewa na Chuo kikuu cha Sokoine cha kilimo (SUA) na chuo kikuu cha Dar es salaam (UDSM) na kuelekea katika azma ya kutekeleza dira ya maendeleo ya taifa 2000-2025. Japo serikali imefanikiwa katika kuzalisha wahandisi wa kilimo na umwagiliaji kwa wingi tangu mwaka 2014 hadi sasa, lakini wanaotumika ni wachache sana ukilinganisha na mahitaji ya wataalam hao ,mfano halmashauri nyingi nchini zina upungufu wa wataalam katika fani ya Uhandisi wa kilimo na umwagiliaji

ambako ndipo panahitaji wataalam wa kusaidia na kuongoza miradi ya umwagiliaji, kutoa elimu kwa wakulima kuhusu umuhimu wa umwagiliaji ,utumiaji wa teknolojia ya umwagiliaji kwa njia ya matone (Drip irrigation system) na utunzaji wa skimu za umwagiliaji.

Ushauri

- i. Serikali kupitia wizara ya kilimo inatakiwa kuajiri wahandisi wengi wa kilimo na umwagiliaji na kuwapeleka katika halmashauri zote nchini ili kufikia lengo la Tanzania ya Viwanda 2000-2025. Maana miradi mingi ya umwagiliaji ipo katikawilaya/ halmashauri.
- ii. Serikali kupitia wizara ya kilimo itoe mafunzo mbalimbali kwa wahandisi wa kilimo na umwagiliaji hasa katika mabadiliko ya teknolojia ya umwagiliaji ili kuendana na mabadiliko hayo.
- iii. Serikali kupitia wizara ya kilimo kuajiri wataalam wa stashahada (Diploma) wenye fani ya umwagiliaji ili wakasaidiane na wahandisi wa shahada za kilimo na umwagiliaji, angalau uwiano wa 1: 4 (mhandisi mmoja na technician 4).


Tume ya umwagiliaji

►Kwa mujibu wa sera ya umwagiliaji 2010 , serikali kupitia wizara ya kilimo iliazimia kuanzishwa kwa tume ya taifa ya umwagiliaji ambayo baadae ilianzishwa, kuanzishwa kwa tume hii ilikuwa ni kufungua uwanda mpana wa kuhakikisha kilimo kinasonga mbele na kutoka kilimo cha kutegemea mvua kwa miaka mingi na kwenda kilimo cha kisasa cha umwagiliaji, japo wizara ilionesha jitihada lakini ilikwama katika muundo wa tume ya umwagiliaji na pia Uwezeshwaji wa miradi mipya na ufufuaji wa miradi ya zamani iliyotelekezwa.

Muundo wa tume ya taifa ya umwagiliaji uliishia hewani na si kwenye mzizi wa tatizo, tume ya umwagiliaji iliyovunjwa na waziri mkuu katika bunge la bajeti 2019/2020 , muundo wake wa uongozi ulianza kwa Mkurugenzi wa tume na kuishia katika kanda za umwagiliaji(zonal irrigation) jambo ambalo halikuwa sahihi na kupelekea mikwamo mingi katika miradi ya umwagiliaji. serikali kushindwa kutoa fedha za kutosha katika miradi ya umwagiliaji na tume kupewa bajeti kiduchu katika kutekeleza miradi yake.

Ushauri

- i. Muundo wa tume ya umwagiliaji ubadilike , muundo wa tume uwe kama ilivyo kwenye barabara(TANROADS) na tume nyingine zenye miundo ya hivyo, muundo wa tume unatakiwa uanzie kwa Mkurugenzi na kufika wilayani , katika mikoa na wilaya tume ya umwagiliaji ijitenge isiwe ndani ya idara ya kilimo, sababu inapokuwa ndani ya idara ya kilimo inashindwa kufanya kazi zake hasa ukizingatia wakuu wa idara wengi wanakuwa sio wahandisi wa kilimo au umwagiliaji hivyo kupelekea mambo kukwama katika umwagiliaji.



- ii. Tume wanapokuwa kwenye upembuzi yakinifu wa mradi na uandaaji wa michoro washirikiane bega kwa bega na mkoa husika na muhimu zaidi wilaya au halmashauri ambapo mradi utatekelezwa , wahandisi wa sehemu husika wakishirikishwa zoezi litakuwa rahisi na kupunguza migongano ya kimaslahi katika Utekelezaji wa miradi na lazima itambulike wahandisi wa kilimo na umwagiliaji wawe chini ya tume na sio wizara ya kilimo ili kuondoa migongano katika kazi , kwani wahandisi wote ni sawa wamesoma masomo yaleyale kinachowatofautisha ni eneo la kazi tu(mfano mhandisi A yuko makao makuu ya tume na mhandisi B yuko wilayani/halmashauri).
- iii. Tume iwashirikishe wananchi/wakulima moja kwa moja katika ujenzi wa miradi na kutoa elimu ya kutosha katika utunzaji wa miradi na faida za kilimo cha umwagiliaji na kuacha kutegemea mvua.
- iv. Tume ifufue miradi iliyokufa na kuifanya ifanye kazi kwa kutoa elimu kwa wananchi/wakulima kwani elimu kwa wakulima ndio msingi wa mafanikio ya miradi ya umwagiliaji .
- v. Serikali ishirikiane vyema na wadau wa maendeleo kama JICA na kutoa sehemu ya fedha inayotakiwa katika kutekeleza miradi bora na imara (value for money)
- vi. Upembuzi yakinifu uzingatiwe katika utekelezaji wa miradi kwani kutofanya hivyo miradi haitadumu na mingi itaharibika mapema sababu sio imara , ni bora kuwa na miradi michache imara na sio miradi mingi isiyo imara.
- vii. Serikali kama ilivyofanya kwenye barabara (TANROADS) na umeme (REA) Inatakiwa ianzishe mfuko wa umwagiliaji kwa kuweka tozo katika bidhaa ambayo itaona nafaa ili kuhakikisha pesa ya kutosha inapatikana ya kujenga miradi imara ya umwagiliaji.

2.0 Utumiaji wa zana za kilimo (Mechanization)

Wizara ya kilimo ina kitengo cha mechanization, lakini kimekuwa hakionekani katika ufanisi wa kazi hii inaweza sababishwa na sababu mbalimbali za kifedha na uteandaji kwa kiasi kikubwa wakulima hawafaidiki na hiki kitengo katika wizara ya kilimo.

Kwa mujibu wa sera ya kilimo ya mwaka 2013, wakulima wapatao asilimia 64 wanatumia jembe la mkono na asilimia 24 wanatumia majembe ya kukokotwa na wanyama kama ng"ombe na asimilia 12 tu ndio wanatumia zana za kisasa kama trekta.

Sababu kubwa ya kuwepo kwa matumizi kidogo ya zana za kisasa za kilimo ni hali duni ya wakulima wengi wa Tanzania ,ambao wamekuwa wakilima miaka nenda miaka rudi lakini maisha yao hayabadiriki sababu wanatumia teknolojia duni ya jembe la mkono,ambayo huwawezesha kulima eneo dogo na kupelekea kupata mavuno kiduchu yanayokidhi mahitaji ya chakula na kuuza kiasi cha mazao kwa ajili ya kujipatia kipato cha kusomesha watoto na kuendesha familia lakini sio kufanya maendeleo tarajiwa.

Pia kwa maeneo wanaobahatika kupata zana za kisasa za kilimo hushindwa kupata msaada wa kitaalam kuhusu mitambo ya kilimo inapoharibika pia matumizi sahihi ya mitambo hiyo ya kilimo.

2.1 Maoni/Ushauri

Serikali kupitia wizara ya kilimo inatakiwa kuendeleza juhudi za kuwafanya wakulima waondokane na jembe la mkono ambalo ni chanzo cha kukifanya kilimo nchini kuendelea kudumaa bila kupiga hatua kwa sehemu kubwa,juhudi hizo nazipongeza kama ambavyo serikali imeingia mkataba na kampuni inayounganisha matrekta ya URSUS pale kibaha.

Ushauri

- i. Wizara ya kilimo na wizara ya viwanda iangalie namna matrekta ya URSUS yatakavyo wafikia walengwa ambao ni wakulima wa hali ya chini na sio matrekta kuangukia mikononi mwa watu wachache ambao sio wakulima, hivyo basi serikali ifanye tathmini Je? Matrekta ya URSUS yamewafikia walengwa

ambao ni wakulima wengi kama wanavyotajwa katika sera ya kilimo ya mwaka 2013.

- ii. Serikali kupitia wizara ya kilimo ikopeshe wakulima wa vijijini zana za kilimo au iwezeshe sekta binafsi ambazo zitakuwa na jukumu la kukopesha wakulima huku serikali wakibeba dhamana.
- iii. Wizara ya kilimo ipeleke wataalam wa agro-mechanization wenye kiwango cha diploma maeneo ya vijijini ili wawe jirani na wakulima katika kutoa msaada wa kitaalam katika matumizi ya zana za kisasa za kilimo
- iv. Wizara ya kilimo iboreshe mazingira ya chuo cha kilimo Mlingano-Tanga ili kiweze kutoa wataalam wengi wa agro-mechanization kwa kiwango cha stashahada ambao watatumika vijijini
- v. Wizara ya kilimo iajiri wakufunzi wa fani ya uhandisi kilimo na kuwapeleka chuo cha Mlingano ili kukidhi mahitaji ya kuandaa wataalam wa kiwango cha stashahada wa kutosha ili angalau uwiano wa 1:4 ufikiwe.

3.0 Ushirika (Cooperatives)

Ushirika ni moja ya nyanja ambayo itawezesha wakulima waweze kujikomboa katika umaskini na kuanza kuonja matunda ya kilimo. Wizara inafanya jambo jema kusisitiza ushirika kwa wakulima hasa katika baadhi ya mazao kama kahawa, korosho, tumbaku nk.

Wizara ya kilimo inatakiwa waende mbali zaidi na kuboresha vyama vya Ushirika kuanzia ngazi ya kijiji, na kuondoa ushirika wa zao moja moja bali ushirika wa wakulima bila kujali ni aina gani ya zao.

3.1 Maoni/Ushauri

- i. Vikundi vya ushirika viundwe kuanzia vijijini kwa msaada wa wataalam wa ushirika, kila kijiji nchini kiwe ni kikundi cha ushirika na kitumie jina la kijiji husika kutambulika kama kikundi cha ushirika
(mfano. Kwedikwazu village cooperative, wilaya ya Handeni, Mkoa wa Tanga).
Hivi vikundi vya ushirika katika vijiji vitaunda kata (mfano msata ward cooperative, hapa vijiji vya kata ya msata vitaunda moja kwa moja ushirika wa kata), ushirika ukitoka kata unaenda wilaya (mfano utaitwa Handeni district

cooperative) na hatimaye kimkoa (mfano Tanga region cooperative)

Jambo la msingi ni kuwa kuanzia kata hadi mkoani kuwe na muundo tofauti na kwenye vijiji,

Mfano, **Kijiji** – wakulima wote katika kijiji watakuwa wajumbe wa ushirika Wakiwa ni wakulima wanaotambulika wenye mashamba ya kumiliki au kukodi, wakulima/wajumbe wote watachagua viongozi ambao ni mwenyekiti ,katibu na mweka hazina

Kata- viongozi wote 3 wa kijiji(mwenyekiti,katibu na mweka hazina) watakuwa wajumbe wawakilishi katika baraza la ushirika la kata,katika kata mwenyekiti atachaguliwa kutoka viongozi wajumbe toka kwenye vijiji , katibu wa ushirika awe ni mwajiriwa wa serikali , na mweka hazina awe ni mwajiriwa wa serikali.

Baraza la ushirika kata ndilo liwe baraza kuu la maamuzi na la kujadili na kupitisha agenda zilizotoka katika mabaraza ya ushirika ya vijiji.

Wilaya – Hapa wawepo wataalam tu wa kufuatilia,kutoa ushauri,kufanya tathmini ya maendeleo katika ushirika ngazi ya kata na vijiji na hatimaye wilaya kupeleka mkoani na kutoka **mkoani** hadi **wizarani** ,lakini mkoa na wizara wawe na mamlaka ya kwenda kwenye kata au kijiji kama kuna jambo linahitaji utatuzi.

- ii. Serikali au wizara kwa kufanya hivyo watakuwa na takwimu sahihi za vijiji ambavyo ni ushirika,kutambua Idadi ya wakulima wote nchini hasa vijijini na kutaiwezesha serikali kupanga maendeleo kwa kuwa na takwimu sahihi za wakulima
- iii. Kujiunga ushirika kwa wakulima iwe lazima bila gharama yoyote , serikali kupitia wizara ya kilimo isaidie michakato yote ya kuanzishwa vijiji vya ushirika na kutoa elimu kwa wakulima mara kwa mara
- iv. Kupitia vijiji vya ushirika serikali na wizara ya kilimo ikopeshe kila kijiji trekta (hasa matrekta ya URSUS) , wawezeshwe zana nyingine za kisasa za kilimo,pembejeo za kilimo kama

mbolea,mbegu n.k ziende moja kwa moja katika kata na kusambazwa kwenye vijiji (baada ya kuwa yanafanyika haya mazoezi ya kugawa zana za kilimo na pembejeo , wilaya husika wanafatilia na kutathimini kama zoezi linatekelezwa ipasavyo)

- v. Wakati wa mavuno ushirika wa kijiji unakuwa na jukumu la kuhakikisha wakulima wanaohitaji kuuza mazao yao wanayakusanya na kupelekwa kwenye soko la ushirika la kata ambapo wanunuzi/wafanyabiashara watakuwa wananunua mazao katika soko la ushirika la kata , na serikali idhibiti mkulima yeyote asiruhusiwe kuuza mazao yake holela katika kijiji na iwe ni marufuku mfanyabiashara yeyote kununua mazao katika kijiji ila katika soko la ushirika tu.
- vi. Kwa kufanya hivyo wakulima watakula matunda ya kazi zao na kuwakwamua na umaskini pia tutazuia madalali ambao wao wananufaika zaidi kuliko wakulima wenyewe.

Umasikini katika taifa husababishwa na kushindwa kwa uzalishaji wa kiwango cha kutosha katika mahitaji muhimu ya wananchi (mfano chakula,nguo n.k) lakini vilevile uzalishaji unaendana sambamba na upatikanaji wa soko la uhakika ndio maana China na nchi za magharibi imeligeuza bara la afrika kama dampo la kuuzia bidhaa zao.

CASE STUDY: CHINA NI NCHI ILIYOKUWA KAMA TANZANIA NA IKAFANIKIWA KWENYE MAPINDUZI YA KILIMO NA HATIMAYE KUWA CHINA YA VIWANDA.

SEHEMU YA PILI

1. SERA NA MIKAKATI YA MAPINDUZI YA VIWANDA NCHINI CHINA.

Sehemu hii ya pili najaribu kufanya uchambuzi na kuchagiza mchango wangu katika **MAREKEBISHO YA SERA YA KILIMO YA MWAKA 2013**, mchango/ushauri/maoni ambao nimeutoa sehemu ya kwanza, sehemu hii najaribu tu kuelezea wenzetu china walipotoka na walivyofanikiwa katika **KILIMO** na kupelekea mapinduzi ya viwanda ,kama sisi tunavyotamani hayo mafanikio.

Mapinduzi ya viwanda china ya sasa yalianza miaka 40 iliyopita wakati wa utawala wa Rais Deng Xiping , wataalam wa uchumi ,wana sayansi na wana zuoni mbalimbali huyatazama kama mapinduzi yenye kasi ya ajabu , tangu mapinduzi ya viwanda nchi za Ulaya miaka 250s iliyopita.

Mapinduzi haya ya viwanda nchini china ,hayakuja hivihivi kwa kutamka tu ,bali mojawapo ya sababu kuu ya mapinduzi haya ni china kugundua wao ni taifa lenye watu wengi duniani,hivyo wana rasilimali watu na nguvu kazi kubwa zaidi ya kuzalisha malighafi zitakazoweza kutumika viwandani.

China waligundua , chini ya asilimia 10 ya wakazi wote duniani wameshafanya mapinduzi ya viwanda na nchi hizi nyingi zilikuwa nchi za Ulaya na Marekani. China wakagundua kama wao wakifanikiwa katika mapinduzi ya viwanda itaongeza asilimia zipatazo 20 katika mapinduzi ya viwanda duniani na hivyo dunia kuingia katika utawala mpya wa teknolojia na viwanda.

Ukuaji wa uchumi na mapinduzi ya viwanda nchini china ,ulizishangaza nchi nyingi duniani hasa mataifa ya Ulaya na Marekani wakiwemo wana uchumi wakubwa duniani, walijiuliza maswali mengi ya kinadharia yasiyo na majibu , moja ya swali hilo ni “ **inakuwaje nchi yenye watu wapatao bilioni 1.4 kutoka kwenye kilimo kisicho na manufaa na kuwa nchi ya viwanda**” wakati nchi

nyingi ndogondogo zenye watu wachache na eneo dogo zimeshindwa kufanya mapinduzi ya viwanda japo zina mazingira mazuri na yenye kushawishi ukuaji wa uchumi.

Kutokana na ukuaji wa china kiuchumi na mapinduzi ya viwanda kuwashangaza wana uchumi wengi duniani wengi walikuwa na maoni tofauti , lakini maoni hayo yaliegemea pande kuu mbili,

Moja “ **Wapo waliioina china kama serikali kubwa sana ,ambayo haiko imara na ingesambaratika kwa sababu haikuwa na demokrasia ya kimagharibi,hakuna haki za binadamu,hakuna uhuru wa kuzungumza,hakuna utawala wa sheria,hakuna mifumo ya kimagharibi katika utawala,hakuna masoko mazuri yaliyopangiliwa,hakuna benki binafsi, hakuna ulinzi wa maandiko ya wataalam/wasomi(intellectual properties), hakuna uwezo wa kufanya ugunduzi zaidi ya kukopi na kuiba teknolojia ya nchi za magharibi na biashara za siri, haimiliki vitu vingi dhidi ya nchi ya magharibi ambazo zimemiliki kwa karne nyingi**” kwa mtazamo huu wachambuzi wengi wa uchumi baada ya uhuru 1949, waliiona china kama taifa litakaloporomoka muda wowote kama ilivyokuwa huko nyuma.

Kundi la pili, lilikuwa na mtazamo huu kuhusu china “**kundi hili liliona ukuaji wa china na mapinduzi ya viwanda umetokana na historia yake ya vizazi na vizazi na kuhusisha na tawala zake za kifalme huko nyuma, kwa mujibu wa historia, china ilikuwa taifa tajiri na kubwa na taifa la kwanza kustaaribika kwa kuwa na mifumo iliyoeleweka kuanzia miaka ya 200K.K hadi 1800K.K, kundi hili linafikiri ilikuwa ni suala la muda tu china kurudisha hadhi yake tukufu ya kutawala tena dunia**” maono ya kundi hili la pili yanapata mkazo na msisitizo kupitia kauli ya mfalme wa Kifaransa enzi hizo (King Napeleon Bonaparte) alivyosema, nanukuu “**Let china sleep for a while, when the dragon awakes, she will shake the world**” mwisho wa kunukuu.

Japokuwa ,makundi hayo mawili yalikuwa na mitazamo yao katika maono,lakini yanachagizwa na u sirias katika uchambuzi wa kiuchumi, badala ya kutegemea katika upande wa historia na mawazo ya kufikirika, wachumi waliendelea kujjuliza hili swali “**inakuwaje nchi isiyo kuwa na biashara zinazoeleweka na ufanyaji tafiti /ugunduzi kuwa na uwezo wa kukua kiuchumi na kufikia digit mbili kwa mwaka, mfululizo kwa miongo mingi na kufanya mabadiliko yenyewe kwa muda mfupi, kutoka uchumi wa kilimo kisicho na tija hadi kuwa ngome ya mapinduzi ya viwanda**”

Wana uchumi wakubwa ,duniani waliendelea kujiuliza, kama ni suala la utamaduni na mahusiano ya jamii za kale zilizoanza kustaarabika mapema, Je Kwanini?, nchi kama Misri,Ugiriki na Dola la Ottoman(uturuki) wameshindwa kufikia hatua hiyo kwa muda mchache kama china?. Swali hili limekuwa gumu sana kupata ufumbuzi juu ya mapinduzi makubwa ya viwanda nchini china.

2.0 NAMNA CHINA WALIVYOFANIKIWA KUTUMIA KILIMO NA KUWAFANYA WAFANYE MAAJABU MAKUBWA KATIKA MAPINDUZI YA VIWANDA.

Historia ya China kushindwa katika mapinduzi ya viwanda kati ya mwaka 1860 hadi 1978.

China imejaribu zaidi ya mara nne hadi kuja kufanikiwa katika mapinduzi ya viwanda kwa zaidi ya miaka 120, kupitia nyakati tofauti tofauti za utawala kabla ya kupata uhuru kamili 1949.

Jaribio la kwanza

Ilikuwa kati ya mwaka 1861 na 1911, jaribio hili lilishindwa vibaya kwani baada ya china kushindwa katika vita na Uingereza mwaka 1860, katika vita iliyoitwa “*Second opium war*” baada ya vita hiyo china ililazimishwa kuingizwa katika mikataba inayozibeba nchi za Ulaya magharibi katika viwanda vyao.

Ufalme wa Qing,ambao ndio ulikuwa unatawala china yote na uliokuwa unafanya jitihada za mapinduzi ya viwanda kupitia uchumi wa kilimo, kujenga meli za kisasa na mfumo wa viwanda ulirudi nyuma kwa kasi kubwa. Miaka 50 baadae juhudi za China kuwa taifa la viwanda zilifika kabisa, na serikali kubaki na madeni makubwa.

Jaribio la pili

Mapinduzi ya viwanda nchini China ,baada ya matumaini kupotea kabisa ,lilizuka vuguvugu la mabadiliko ya kisiasa,yaliyofatiwa na machafuko ndani ya jamii na mwisho wa siku kupelekea mapinduzi yaliyoitwa Xinhai (*Xinhai Revolution*) mnamo mwaka 1911.

Hii ilipelekea kuuvunja utawala wa kifalme (Qing Monarchy) na kuanzishwa rasmi Jamhuri ya China (Republic of China), serikali ya kwanza ya china iliyokuwa na mifumo na muundo wa kimagharibi. Jamhuri mpya ya china ilijaribu kurudisha matumaini ya mapinduzi ya viwanda kwa kukopi mfumo wa Marekani wa **“Political institution”**, kwa kuingiza mambo ya demokrasia na mgawanyo wa madaraka (bunge, serikali na mahakama).

Katika kipindi hiki kauli mbiu maarufu miongoni mwa wachina ilikuwa **“ Ni sayansi na demokrasia pekee vitaisaidia China”**, wana mapinduzi wasomi waliamini utawala wa kifalme umeshindwa kufanya mapinduzi ya viwanda na kuirudisha China nyuma na hii ilitokana na kukosekana demokrasia na ushiriki wa kisiasa (kama Nadharia hii ya kimagharibi ya political institution inavyosema).

Japo wana mapinduzi wasomi ,waliamini katika misingi na nadharia za kimagharibi, toka mwaka 1911 ya Xinhai Revolution, miaka 40 baadae china iliendelea kubaki kuwa nchi maskini duniani.

Hali hii ilipelekea mavuguvugu mbalimbali ,ikiwemo kutaka China huru kutoka koloni la Uingereza kupitia Japan na ilipofika mwaka 1949, Jamhuri ya China ilishindwa vibaya na jeshi la wakulima wakomunist (Communist peasant army) na kuundwa Jamhuri ya watu wa china .

Jaribio la tatu

Mapinduzi ya viwanda nchini china ,serikali mpya iliingia na hali ya kusahihisha makosa ya serikali zilizopita katika mapinduzi ya viwanda , kipindi hiki serikali ya China iliamua kukopi sera za shirikisho la kisovieti (USSR) kwa kutumia mpango uliojulikana kama **“ Central Planning Model”** , miaka takribani 29 ilipita tena ,lakini mpango wa kuifanya china ya viwanda ulishindwa tena.

Mnamo mwaka 1978, china ilibakia katika umaskini mkubwa tu huku pato la taifa likiwa halitofautiani sana na kipindi cha mwaka 1860 wakati wa vita kati ya China na Uingereza iliyojulikana kama **“second opium war”** .China ilishindwa katika harakati za mapinduzi ya viwanda kwa vipindi vitatu tofauti mfululizo ambavyo vinaleta zaidi ya miaka 120.

SWALI, Ni Kwanini ni nchi nyingi zilishindwa katika mapinduzi ya viwanda ikiwemo China?

JIBU , kutokana na nadharia (theory) ya *utaasisi*(institutional) inasema nchi nyingi zilishindwa kwa sababu ya kutokuwa na **taasisi madhubuti** za usimamizi na pia uwepo wa **vikwazo kwa wasomi/wataalam kuingiliwa na wanasiasa**(maamuzi mengi kuwa ya kisiasa na sio kufuata ushauri wa kitaaluma), **uwepo wa soko huria**(nchi maskini haipangi bei katika soko la dunia bali hupangwa na mataifa yenye nguvu tayari ya kiuchumi na viwanda), na **biashara huria**(serikali nyingi kushindwa zilishindwa kudhibiti biashara), hizo ni moja ya sababu zilizopelekea nchi nyingi kushindwa katika mapinduzi ya viwanda japo sababu zinaweza kuwa nyigi .

►Katika historia ya mapinduzi ya viwanda Uingereza huchukuliwa kama mapinduzi makubwa ya viwanda katika historia ya kiuchumi kwa binadamu, japokuwa mapinduzi katika historia yalianzia katika moto na kilimo,kabla ya mapinduzi makubwa ya viwanda kufikiwa.

Kuanzia mwaka 1760, maisha ya wananchi nchini Uingereza yalianza kubadilika na kuwa maisha mazuri na hii kupelekea kila nchi duniani kujaribu kufanya mapinduzi ya viwanda kama ilivyokuwa Uingereza.

Nchi chache sana ndizo zilizofanikiwa, mathalani nchi za Amerika kaskazini na Ulaya magharibi ,Japan na nchi baadhi za bara Asia ambazo ni Asian tigers (Singapore,Taiwan na Korea kusini) nchi hizi zimefanikiwa sana katika mapinduzi ya viwanda baada ya Uingereza na nyingine zimeipita Uingereza mfano Marekani.

Je? Kulikuwa na utofauti gani katika jaribio la nne kuitafuta China ya viwanda.

Jaribio la nne

Mapinduzi ya viwanda nchini China, mnamo mwaka 1978 chini ya Uongozi wa **Rais Deng Xiaoping**, China ilikataa kuchukua ushauri kutoka kwa washauri wa uchumi wa nchi za magharibi (tofauti na Urusi walivyofanya miaka ya 1990s), badala yake China iliamua kukaa chini na kubuni mbinu ya kutimiza ndoto yao ya viwanda kwa kuangalia mazingira yao wenyewe kwa kuwachukua wahitimu wa vyuo vikuu, kufanya majaribio ya kutengeneza uchumi.

Mpango (blue print) uliotumika katika kufikia mikakati hiyo ni kama ifuatavyo;

1. Kuendeleza na kusimamia hali ya kisiasa isiyumbe kwa gharama zozote zile (political stability)
2. Kujielekeza katika tabaka la chini kabisa ili kufanya mageuzi (walianza na sekta ya kilimo hasa vijijini)
3. Kuhamasisha viwanda vijijini japokuwa ilitumika teknolojia ya kizamani
4. Kutumia bidhaa zinazozalishwa na viwanda vidogo vidogo
5. Serikali kutoa msaada mkubwa katika ujenzi wa miundombinu itakayorahisisha usafirishaji wa bidhaa zinazolishwa vijijini na kufika kwenye masoko.
6. Kufuata mfumo wa pamoja wa serikali na sekta binafsi badala ya mfumo wa ubinafsishaji na kupelekea ukuaji wa viwanda kutoka viwanda vidogo hadi viwanda vikubwa, kutoka kutumia nguvu bila tija hadi kufanya uzalishaji wenye tija, kutoka kuzalishwa bidhaa hadi kutengeneza mitaji mikubwa ya kifedha na mwisho kutoka taifa la kutunza hadi taifa la kutumia ili kupanua wigo wa uchumi kukua.

Jaribio la nne, kwa China kuitafuta China ya viwanda ilikuwa na fomula ya siri **“secret recipe”** waliyotumia Uingereza katika mapinduzi ya viwanda, japokuwa China walitumia njia tofauti katika utaasisi (political institution), China iliamua kubaki taifa lenye mamlaka juu ya kila kitu ili kufanikisha azma yake ya mapinduzi ya viwanda.

Uingereza

Mapinduzi ya viwanda nchini Uingereza yalifuata njia zifuatazo;

1. **1600-1760, Proto-industrialization**- Hii ni awamu iliyotumika kuendeleza viwanda vya maeneo ya vijijini (Viwanda ambavyo vilitegemea malighafi za kilimo) pia kufanya biashara na wafanyabiashara wanaotoka maeneo ya mbali ili kukuza soko.
2. **1760-1830, First industrial revolution** –Hii awamu ilibeba dhana ya kuzalishwa bidhaa nyingi kwa ajili ya soko kubwa (bidhaa nyingi zilitokana na kilimo).
3. **1830-1850, Industrial trinity boom**- Hii awamu ilibeba dhana kuu tatu ambazo ni kusambaza nishati, Usafirishaji na miundominu itakayotumika kufikisha bidhaa katika masoko.
4. **1850-1900, Second industrial revolution**- Hii awamu ilihusisha muunganiko wa uzalishaji wa kiwango kikubwa wa bidhaa ukienda sambamba na uzalishaji wa kiwango kikubwa wa zana za kilimo.
5. **1900 na kuendelea, Welfare stage**-Hii awamu ilihusisha masuala ya uchumi kama vile , huduma za kisasa katika kukuza uchumi, bima ya kukosa ajira, usawa katika upatikanaji huduma za afya na elimu, upatikanaji wa vyandarua kutunza afya za wananchi na magonjwa kama malaria , na mwisho ni utulivu wa kisiasa kwa kuzingatia demokrasia,haki za binadamu, haki ya kupiga kura,haki za msingi mfanyakazi anapofia kazini n.k.

Hizo ni njia na awamu ambazo Uingereza ilizitumia katika mapinduzi ya viwanda ,ambazo China iliziboresha kuendana na mazingira yao ,hali iliyopelekea kuyafikia mapinduzi ya kiuchumi waliyo yasotea kwa zaidi ya miaka **120** lakini China katika jaribio la nne walitumia muda mchache

sana kufanya mapinduzi ya kilimo na Viwanda ambapo ni zaidi ya miaka 40 iliyopita.

Marekani

Njia ilizotumia Marekani katika mapinduzi ya viwanda.

1. **Kabla ya 1820:** Awamu ya kusambaza viwanda vijijini nchi nzima (malighafi ilikuwa mazao ya kilimo).
2. **1820-1860: First industrial revolution**— Awamu ya uzalishaji mkubwa wa nguo ulioegemea katika kuagiza au kuiba teknolojia ya Uingereza.
3. **1830-1870: Boom in industrial trinity**, -Hii ni awamu iliyojidhatiti katika nishati, usafirishaji na utengenezaji miundombinu.
4. **1870-1940: Second industrial revolution**—Hii awamu ilibeba dhana jumishi au shirikishi katika uzalishaji mkubwa wa chuma, magari, mawasiliano, madawa na kufanya mapinduzi ya kilimo katika kutumia mashine za kulimia, umwagiliaji na uvunaji.
5. **1940s-hadi leo: Entering the welfare state** – Hii awamu iliingwa baada ya vita kuu ya pili ya dunia kwa kutambua haki za raia - haki ya kupiga kura, haki za wanawake, n.k

Mapinduzi ya viwanda China

Baada ya China kufanya upembuzi yakinifu katika mikakati niliyoeleza huko juu, hatimaye ikagawanya mpango wake uliokamilika katika awamu kuu tatu, awamu hizo ni kama zifuatazo;

China iliachana na njia ilizokuwa ikizitumia hasa za Marekani kwa muda wa miongo inayokaribia mitatu. Njia iliyotumia katika mapinduzi ya viwanda na kufanikiwa iligawanyika katika njia kuu tatu.

1. **1978-1988: Proto-industrialization.** –Awamu hii ilitumika kuunganisha na kushirikisha katika kuendeleza juhudi za vyama vya ushirika vilivyofunguliwa vijijini badala ya kushughulikia na mkulima mmoja mmoja, njia hii ilitumika nchi nzima, hivi vyama vya ushirika, zilikuwa kama injini ya ukuaji uchumi katika awamu ya kipindi cha miaka 10 ya kutengeneza uchumi wa viwanda. Vyama vya ushirika katika vijiji viliongezeka maradufu kutoka million 15 hadi Milioni 18.9. hali hii ilipelekea kukua kwa

pato la jumla katika vijiji kutoka asilimia 14 hadi asilima 46,wakulima wanaozalisha na wafanyakazi walifikia Milioni 100 mnamo mwaka 1988, ujira wa jumla kwa wakulima uliongezeka mara dufu. Kutokana na ongezeko hili katika mahitaji ya msingi ya binadamu(nyama,Chakula ,nguo n.k) China ilifanikiwa sana ,na katikati ya miaka ya 1980s, china iliweza kumaliza tatizo la Chakula nchini humo

Katika awamu hii zaidi ya wakulima milioni 800 walinufaika na mabadiliko haya ya sera za kiuchumi katika kutafuta mapinduzi ya viwanda.

2. **1988-1998: First industrial revolution.** Awamu hii ilijikita katika uzalishaji mkubwa hasa katika bidhaa ambazo zinawagusa wananchi wengi nchini china katika maeneo ya vijijini na mijini na vilevile kujikita katika uagizaji wa mashine za kilimo kutoka nje. Katika kipindi hiki China ikawa mzalishaji na muuzaji mkubwa duniani wa nguo,muagizaji na muuzaji mkubwa wa pamba, pia mzalishaji na muuzaji mkubwa samani za ndani na midoli mbalimbali. Katika kipindi hiki vyama vya ushirika vijijini viliendelea kukua kwa kasi na kazi zake kufikia asilimia 30 ya nguvu kazi katika vijiji vyote. Viwanda vya vijijini vilikuwa kwa asilimia 28 kwa mwaka, na kukua mara mbili kila baada ya miaka mitatu kati ya mwaka 1978 hadi 2000.
3. **1998-hadi leo: Second industrial revolution.** Awamu hii,ilishirikisha uzalishaji mkubwa bidhaa unaoenda sambamba na uzalishaji mkubwa wa mashine mbalimbali. Kutokana na ongezeko hili ilipanua soko la ndani kwa bidhaa za kiwango cha kati,kupanuka kwa sekta ya usafirishaji, uhitaji mkubwa wa makaa ya mawe,chuma,simenti,madawa,ujenzi wa miundombinu ,meli n.k , kwa ujumla zaidi ya maili milioni 2.6 (km milioni 4.2) za barabara za lami zilijengwa,zikiwemo maili 70,000 (km 112,000) za barabara kubwa za njia tatu hii ni sawa na zaidi ya asilimia 46 ya barabara za Marekani. Majimbo 28 kati ya majimbo 30 yameshaunganishwa na miundombinu ya treni za umeme yenye urefu wa maili 10,000(km 16,000), ambayo ni sawa na Asilimia 50 zaidi ya jumla ya urefu wa njia za treni dunia nzima kwa nchi zenye miundombinu hiyo.

Mafanikio ya China katika soko la ndani na kimataifa.

Swali ambalo tunatakiwa tujiulize je? China imefanikiwa katika soko la bidhaa zake baada ya kufanikiwa katika mapinduzi ya viwanda? Jibu ni **NDIYO**

1. China ilitoka soko la ndani na nje hasa bara la Afrika na Latin America ,sababu ilitengeneza bidhaa zilizovunja soko la nchi za Ulaya na kufanikiwa kushinda.
2. Alisimamia nidhamu katika uongozi wa makampuni yake na kuwa mwepesi katika kuiga teknolojia za magharibi.
3. China alitengeneza mfumo wa **Darwinin** , katika kutengeneza panapoharibika na kuwaondoa wanaopoteza/kuharibu (watumishi wa serikali wasio waaminifu).

Mapinduzi ya viwanda China leo hayategemei teknolojia pekee ,bali na utafutaji masoko nje ya China , kwa kutumia mbinu ya **“mutually beneficial trade”** tofauti na mbinu inayotumiwa na nchi za magharibi iitwayo **“gunboat diplomacy”** na karata ya kucheza hizi mbinu zote mbili ni katika bara la Afrika ikiwemo Tanzania.

China ya sasa kiuchumi duniani

► Mwanzoni mwa miaka ya 1970, Rais wa Marekani aitwaye Richard Nixon , alipotembelea China , ilikuwa inazalisha bidhaa chache sana kulinganisha na Marekani, lakini ilipofika mwaka 1980 china ilianza kuzalisha bidhaa nyingi sana na kuanza kuushangaza ulimwengu kwa kupiga hatua kubwa katika mapinduzi ya viwanda na ilipofika 2010 ikashika namba katika mapinduzi ya viwanda na kuiacha Marekani kushika namba mbili.

► Miaka 40 , iliyopita pato la mwaka la china lilikuwa ni moja ya tatu (1/3-theluthi moja) ya nchi za kusini mwa jangwa la Sahara ikiwemo Tanzania , lakini leo China ni nchi ya pili duniani kwa kuwa na uchumi mkubwa baada ya Marekani na inayoongoza duniani kwa kuzalisha bidhaa mbalimbali kutokana na mapinduzi ya viwanda yaliyoanzia kwenye **KILIMO**.

- i. Inazalisha asilimia 50 ya bidhaa za viwandani zinazozalishwa duniani kote,miongoni mwa bidhaa hizo ni vyuma(crude steel)-asilimia 50 ya uzalishaji na usambazaji duniani ,
- ii. Simenti(asilimia 60 ya uzalishaji wote duniani),
- iii. Makaa ya mawe(asilimia 50 ya uzalishaji duniani),
- iv. Magari(asilimia 25 ya uzalishaji na usambazaji duniani), na oda za bidhaa mbalimbali toka viwanda vya China zaidi ya asilimia 150 dhidi ya Marekani,
- v. Vilevile China ni mzalishaji mkubwa duniani wa meli,treni za mwendo kasi,roboti,ujenzi wa madaraja, barabara kubwa,madawa,mashine mbalimbali ,kompyuta,simu n.k

► Watu wengi hasa wachumi hufikiria miujiza ya kiuchumi China inafikia mwisho ,kwa sababu ya uchumi wa china kuporomoka kutoka digit mbili hadi digit moja (7%), hii ni kutokana na soko lake duniani kuporomoka na pesa yake kukumbwa na ushindani mkubwa na vita ya kibiashara kati yake na Marekani lakini lazima tutambue ya kuwa Marekani imewahi kuwa n mkwamo huo na mdodoro wa uchumi kwa kipindi cha miaka 15 huko nyuma kwa vipindi tofauti.

Tanzania inajifunza nini kutoka China?

Tumeona China walivyojaribu kufanya mapinduzi ya viwanda iliyowachukua zaidi ya miaka 120,hadi kuja kufanikiwa kwa kuamua kubadilisha mbinu za kuwatumia wasomi wake wenyewe na kuanzishwa program mbalimbali zilizoanzia kweye kilimo na kufikia viwanda vikubwa kabisa.Vile vile tumeona China na mifano ya nchi kama Uingereza na Marekani na mbazo ziliamua kutumia mikakati madhubuti ya kuunda **taasisi imara** za kusimamia mapinduzi ya kiviwanda.

Mfumo wa soko huria ni kikwazo kwa nchi kupiga hatua za maendeleo hasa kutimiza ndoto ya viwanda , Tanzania tuna historia ya **“Tanzania ya viwanda”** toka tupate uhuru , tulianza na viwanda vidogo ,vya kati na vikubwa japo tulianguka ,lakini sasa ni muda wa kusafisha makosa na kuanza upya kama China kwa kuwaamini wasomi wetu ambao watatutengenezea mpango wa siri au wa wazi kufikia Tanzania ya viwanda ambayo ni ndoto ya kila Mtanzania pia

tutumie zaidi soko la ndani na kuliimarisha zaidi ili tunapotoka nje tupeleke bidhaa ambazo zitashindana na soko la nje.

Tumeona namna maendeleo ya uchumi wa viwanda ulivyo na mfuatano ulio sahihi ambao haitakiwi kuruka hatua hata moja , tumeona mapinduzi ya viwanda nchi nyingi yameanzia kwenye mapinduzi ya kilimo hadi viwanda vikubwa.

Hatujachelewa bado na tuna nafasi katika kufikia mapinduzi ya viwanda hata kama ikituchukua miaka 100. Mapinduzi ya viwanda ni kama kujifunza hesabu huwezi kuanza kujifunza hesabu za mlinganyo na aljebra wakati hujui hesabu za kutoa ,kujumlisha ,kugawanya na kuzidisha.

Kama China ilivyoamua kuachana na washauri wa kimagharibi na kukaa chini kutengeneza mpango uliozaa matunda na kuunshangaza ulimwengu na sisi tunaweza kwa kuanzia kwa Rais Magufuli kama China walivyoanzia kwa Rais Deng Xiaoping.

Mungu ibariki Tanzania.

Ndimi, Ayubu Massau (Agric. Eng.)

+255763188907

mbogomasau@gmail.com

Morogoro